



CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI ZA ELIMU YA JUU TANZANIA

S.L.P 35928 DAR ES SALAAM, Tanzania

Simu: 022 2401581, Nukushi: 022 2401582

Tovuti: www.thtu.or.tz Barua pepe: thtuhq@thtu.or.tz

Kumb. Na. THTU/HQ/AD.03/0790.2022

Tarehe: 01/08/2022

Wanachama Wote,
THTU.

YAH: TAARIFA YA UCHAGUZI MKUU WA TAIFA WA THTU WA MWAKA 2022

Husika na kichwa cha habari hapo juu.

Tume ya Uchaguzi ya THTU Taifa inapenda kuwatangazia wanachama wote kwamba Mkutano Mkuu wa uchaguzi wa THTU utafanyika mkoani Tabora siku ya Alhamisi tarehe 22/12/2022.

Uchaguzi utafanyika katika nafasi zifuatazo:

1. Mwenyekiti wa Chama
2. Mratibu Mkuu wa Kamati ya Wanawake
3. Mratibu Msaidizi wa Kamati ya Wanawake
4. Mweka Hazina wa Chama
5. Mwakilishi wa Vijana
6. Mwakilishi wa Wanachama wenye Ulemavu.

Hivyo, Tume ya Uchaguzi inawaalika wanachama wote wenye sifa na uwezo wa kuwa viongozi wa THTU Taifa kuomba kugombea nafasi kama zilivyoainishwa hapo juu. Uchukuaji wa fomu za kugombea utanza tarehe 03/08/2022 na mwisho wa kuzirejesha ni tarehe 19/08/2022. Fomu hizo zitapatikana kwenye tovuti ya Chama, makao makuu ya chama na kwa Wenyeviti/Makatibu wa Matawi. Fomu zitarejeshwa kupitia barua pepe ya chama au makao makuu ya Chama.

Pamoja na tangazo hili, tunaambatisha ratiba na viwango vya ada za fomu kwa wagombea. Aidha, wanachama mnashauriwa kupitia katiba ya chama na kanuni za uchaguzi zinazopatikana kwa wenyeviti wa matawi au kwenye tovuti ya chama.

"NIA NA MWELEKEO WETU DAIMA NI KUJENGA, TAIFA KWANZA"

Mariki H. Reginald

Mwenyekiti - Tume ya Uchaguzi

Nakala:

1. Mwenyekiti THTU, Taifa
2. Katibu Mkuu THTU, Taifa
3. Wenyeviti wa Matawi
4. Msajili wa Vyama Huru vya Wafanyakazi na Waajiri.

RATIBA YA UCHAGUZI WA VIONGOZI WA THTU TAIFA

SN	TAREHE	TUKIO	MUHUSIKA	MAHALI
1.	03/08/2022	Kuchukua Fomu za kugombea	Wanachama	Tawini/makao makuu/tovuti ya chama
2.	09/08/2022	Kuanza kurudisha fomu za kugombea	Wanachama	Makao makuu/email (<i>thtuhq@thtu.or.tz</i>)
3.	19/08/2022	Mwisho wa kurudisha fomu za kugombea	Wanachama	Makao makuu/email (<i>thtuhq@thtu.or.tz</i>)
4.	15 – 16/09/2022	Kupitia fomu za walioomba kugombea	Tume ya Uchaguzi	Eneo litakaloandaliwa na makao makuu
5.	19/09/2022	Kutangaza majina ya walioomba kugombea	Tume ya Uchaguzi	Makao makuu
6.	19/09/2022	Kuanza kupokea pingamizi/rufaa	Katibu wa Tume ya Uchaguzi	Makao makuu/email (<i>thtuhq@thtu.or.tz</i>)
7.	03/10/2022	Mwisho wa kupokea pingamizi/rufaa	Tume ya Uchaguzi	Makao makuu/email (<i>thtuhq@thtu.or.tz</i>)
8.	04/10/2022	Kupitia pingamizi/rufaa zilizowasilishwa	Tume ya Uchaguzi	Makao makuu
9.	03 – 04/11/2022	Mahojiano na wagombea	Tume ya Uchaguzi/wagombea	Dodoma
10.	07/11/2022	Kutangaza majina ya wagombea waliopitishwa	Tume ya Uchaguzi	Makao makuu/tovuti/tawini
11.	01/12/2022	Kuanza kampeni kwa wagombea	Wagombea	Matawini
12.	21/12/2022	Mwisho wa kampeni	Wagombea	-
13.	22/12/2022	Uchaguzi mkuu	Tume ya uchaguzi/wagombea/wanachama	Tabora
14.	23/12/2022 – 05/01/2023	Kupokea rufaa	Kamati ya rufaa	Makao makuu
15.	06/01/2023	Kusikiliza rufaa (kama zipo)	Kamati ya rufaa	Makao makuu
16.	20/01/2023	Kuapishwa viongozi wateule na makabidhiano ya ofisi	Viongozi wateule/mwanasheria wa chama	Makao makuu

VIWANGO VYA ADA ZA FOMU KWA WAGOMBEA (kama ilivyoelekezwa na mkutano wa 11 wa Baraza kuu la chama Taifa wa tarehe 21- 22/12/2021).

SN	NAFASI YA UONGOZI	KIWANGO CHA ADA
1.	Mwenyekiti wa Chama	100,000/=
2.	Mratibu Mkuu wa Kamati ya Wanawake	70,000/=
3.	Mratibu Msaidizi wa Kamati ya Wanawake	70,000/=
4.	Mweka Hazina wa Chama	70,000/=
5.	Mwakilishi wa Vijana	50,000/=
6.	Mwakilishi wa Wanachama wenye Ulemavu.	50,000/=

NB: Ada za kuchukua fomu zitalipwa kwenye Akaunti ya Chama iliyopo Benki ya CRDB.

Jina: **Secretary General – THTU**

Namba ya akaunti: **01J1088667700**

Pay in slip iambatishwe na fomu ya kugombea.